

**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(TAMISEMI)  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO**

SHULE YA SEKONDARI MTITU  
S. L. P 121,  
**IRINGA**  
12/12/2020

KUMB: KDC/MTS/JI/2020/.....

JINA LA MWANAFUNZI.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA  
SEKONDARI MTITU, WILAYA YA KILOLO MKOA WA IRINGA  
MWAKA 2021**

**1. UTANGULIZI**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021, Shule ya sekondari MTITU ipo umbali wa km 13 kutoka makao makuu ya wilaya ya kilolo na km 25 kutoka stand ya Ipogolo-Iringa. Usafiri wa Basi unapatikana kuanzia Ipogolo – Ndiwili kwa nauli ya 2,000/= na kutoka Ndiwili hadi shuleni ni Tsh.3000/=kwa usafiri wa bodaboda.

Muhula wa masomo Unaanza tarehe 11/01/2021, Unatakiwa kuripoti Shuleni tarehe hiyo na mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2021. Usipoiripoti, baada ya tarehe hiyo, hatuaza kisheria zitachukuliwa kwa mzazi kwa kushindwa kuwajibika.

**2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**A. SARE ZA SHULE**

**Wasichana** – sketi (2) rangi ya zambarau upana wa mkanda nchi 2,malinda nane ya kupanga, iwe ndefu kuvuka magoti, mashati (2) meupe mikono mifupi, sox (2) nyeupe, viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba jozi 2 na sweta la kijani

**Wavulana** – Suruali (2) rangi nyeusi malinda mawili kila upande na mkunjo chini (turn up),mashati (2) meupe mikono mifupi, sox (2) nyeupe, viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba jozi 2 na sweta la kijani

**B. SARE ZA MICHEZO** – kila mwanafunzi awe na raba za michezo, nguo za michezo/trucksuit nyeusi yenye mistari nyeupe(wasichana) na bukta nyeusi zenye mistari nyeupe(wavulana).

c. Vifaa vya taaluma – kila mwanafunzi anapaswa kuwa na daftari kubwa (12) kwa kuanzia, karamu za kutosha, rula na mkebe wa hesabu na begi la daftari.

d. Shule hii ni ya kutwa, Serikali inagharimia Elimu, wajibu wa mzazi katika zama hizi za Elimu bila malipo ni kuhakikisha mwanafunzi anakuwa na vitendea kazi darasani, anapata chakula, nauli ya kuja shuleni na kurudi nyumbani, huduma za afya (kadi ya CHF ni muhimu), pesa ya matumizi (pocket money) na mahitaji mengine ya kibinadamu.

### **3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebisha kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995, Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia yafuatayo:

- a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumra ni jambo la lazima.
- b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuri ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
- d. Kuwahi katika kila shughuri za shule na nyingine utakazopewa.
- e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- g. Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa.
- h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
- i. Kutunza mali za umma.

### **MAKOSA YAFUATAYO YANAWENZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE**

- a. Wizi
- b. Uasherati na ushoga
- c. Ubakaji
- d. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadharika.
- e. Kupigana au kupiga
- f. Kuharibu kwa makusudi mali za umma
- g. Kudharau bendera ya Taifa

- h. Kupata mimba au kusababisha mimba
- i. Kuoza au kuolewa
- j. Kutoa mimba
- k. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule na watu
- l. Kukataa adhabu kwa makusudi.
- m. Kuwa na simu ya mkononi

**4. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.**

- a. Aje na nakala (copy) ya cheti cha kuzaliwa.
  - b. Picha (passport)3 zilizopigwa kwenye kitambaa cha bluu nyuma.
  - c. Medical examination form – ijazwe na mganga mkuu wa hospitali ya serikali na itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni
5. Tafadhari soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

**KARIBU SANA MTITU SEKONDARI**

.....  
MAYALA J. MANAMBA  
**MKUU WA SHULE – MTITU SEKONDARI**

**KILOLO DISTRICT COUNCIL  
MTITU SECONDARY SCHOOL**

**TO THE MEDICAL OFFICER,**

.....  
.....

**RE;**.....

Please examine the above named person as his/her fitness to studies in the school;

Eye.....

Ears.....

Chest.....

Spleen.....

Stool.....

Urine.....

Blood.....

**MEDICAL CERTIFICATE**

I have examine the above named person, and considered that;

.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....

Date.....Signature .....

Hospital/Heath Centre..... designation.....